

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**SEHEMU YA MAFUNZO YA UALIMU**

**1 UTANGULIZI**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia sehemu yake ya mafunzo ya Ualimu inasimamia na kutoa mafunzo ya Ualimu kwa vyuo 35 ya Ualimu ya Seilikali na vyuo ya ualimu visivyo ya Serikali. Aidha kwa upande wa vyuo ya Ualimu ya Serikali, Wizara inatoa kozi Za Astashada ya Ualimu elimu Awali na Msingi, Stashahada maalumu ya ualimu sayansi (miaka 3) na Stashahada ya ualimu sekondari (miaka 2).

**2 SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA**

**a. NGAZI YA ASTASHAHADA**

Sifa za jumla za kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Tarajali ngazi ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Msingi ni wahitimu wa Kidato cha Nne wenye ufaulu wa Daraja la I-III. Aidha, sifa za kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Tarajali ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari katika masomo ya Sayansi, Biashara na Hisabati (miaka 03) ni wahitimu wa Kidato cha Nne wenye ufaulu wa Daraja la I-III kwa kiwango cha ufaulu wa kiwango cha "C" katika masomo matatu katika hayo, mawili yawe ni ya tahasusi za masomo ambayo mwombaji anaomba kusomea.

**b. NGAZI YA STASHAHADA**

Sifa za jumla za kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Tarajali ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari ni wahitimu wa Kidato cha Sita wenye ufaulu wa Daraja la I-III kwa kiwango cha "Principal Pass" mbili (02) za masomo yanayofundishwa katika shule za sekondari kidato cha I-IV.

### **3. AINA YA MAFUNZO NA VYUO VINAJVYOTOA MAFUNZO HAYO**

#### **A. MAFUNZO YA UALIMU TARAJALI NGAZI YA ASTASHAHADA YA ELIMU YA AWALI NA MSINGI**

Na.	AINA YA MAFUNZO	VYUO	MUDA WA MAFUNZO
1	Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi	Bustani TC, Ilonga TC, Kabanga TC, Katoké TC Kitangali TC, Kinampanda TC, Mandaka TC Mtwaru (U) TC, Mhonda TC, Murutunguru TC Mpuguso TC, Singachini TC, Tandala TC, Tarime TC, Vikindu TC, Nachingwea TC, Ndala TC, Mamire TC, Shinyanga TC, Marangu TC, Tabora TC, Mbonduli TC, Sumbawanga TC na Dakawa TC	Maka 2
2	Astashahada ya Ualimu Elimu Maalum	Patandi TC, Kabanga TC na Mpwapwa TC	Maka 2

3	Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali	Kinampanda TC, Nachingwea TC, Mhonda TC Tarime TC, Vikindu TC, Mpuguso TC, Mandaka TC, Singachini TC Murutunguru TC, Kabanga TC, Bustani TC Ndala TC, Katoke TC, Bunda TC, Sumbawanga TC, Tabora TC	Maka 2
4	Astashahada ya Ualimu Elimu kwa Mchezo	Tarime TC, Mtwaro (K) TC, Ilonga TC, Tabora TC	Maka 2
5	Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi (English Medium)	Dakawa TC, Marangu TC, Tabora TC	Maka 2

**B. MAFUNZO YA UALIMU TARAJALI NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI MASOMO YA SAYANSI, BIASHARA NA HISABATI**

1	Stashahada ya Ualimu Sayansi, Biashara na Hisabati	Monduli TC, Butimba TC, Kleruu TC, Songea TC, Tukuyu TC, Kasulu TC, Mpwapwa TC, Mbogoro TC, Korogwe TC, Tabora TC Mandaka TC (kwa masomo ya Sayansi na Hisabati) na Sinyanga TC (kwa masomo ya Biashara)	Maka 3
---	--	--	--------

**C. MAFUNZO YA UALIMU KAZINI (ASTASHAHADA YA ELIMU MSINGI ELIMU MAALUMU)**

<b>N<sub>a.</sub></b>	<b>AINA YA MAFUNZO</b>	<b>CHJO</b>	<b>MUDA WA MAFUNZO</b>
1	Astashahada Elimu Maalum (Mafunzo kazini) Msingi	Patandi TC	Maka 2

**D. STASHAHADA YA UALIMU SEKONDARI (MAKA 2)**

1	Stashahada ya Ualimu Sayansi na Hisabati	Monduli TC, Mandaka TC, Butimba TC, Kleruu TC, Songea TC, Tukuyu TC, Kasulu TC, Mpwapwa TC, Mwanga TC, Korogwe TC, Mamire TC na Tabora TC	Maka 2
2	Stashahada ya Sayansi ya Jamii , Biashara na Lugha	Bunda TC, Mtwara (K) TC, Marangu TC, Nachingwea TC, Shinyanga TC, Mandaka TC, Mpuguso TC, Dakawa TC, Butimba TC, Tabora TC, Mwanga TC, Tarime TC, Shinyanga TC,	Maka 2
3	Stashahada ya Ualimu Mchezo, Muziki, Sanaa za Ufundu na Sanaa za Maonesho	Butimba TC	Maka 2
	Stashahada ya Ualimu Mchezo,	Butimba TC , Mtwara TC na Mpwapwa TC	Maka 2